

teuliwa kuwa Katibu Mkuu wa UWT

Ulega atoa neno, Kahama Fresh yasifu Programu BBT

Na MWANDISHI WETU

KAMPUNI ya Kahama Fresh inayomiliki Kiwanda cha kusindika maziwa na shamba la mifugo, imeunga mkono Programu ya BBT kwa kutoa ng'ombe wa maziwa (mitamba) watano kwa kikundi cha vijana 17.

Imeelezwa lengo la kupewa ng'ombe hao ni kuwawezesha kujishughulisha na uzalishaji wa maziwa na kujiongezea kipato.

Kikundi hicho kilikabidhiwa ng'ombe hao jana katika shamba la mifugo la kampuni hiyo lililopo wilayani Karagwe, mkoani Kagera.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega alimpongeza Mkurugenzi wa Kampuni hiyo, Josam Ntangeki kwa kuunga mkono Programu ya BBT kwa vitendo.

"Nampongeza Josam kwa kuunga mkono programu hii ya BBT kwa kuwakopesha ng'ombe wa maziwa vijana wetu kupitia mpango wa Kopa Ng'ombe Lipa Maziwa, kuwawezesha kuzalisha maziwa kwa wingi na kuyapeleka katika viwanda vya uchakataji wa maziwa kikiwemo cha Kahama Fresh," alisema.

Aliongeza kuwa, programu ya BBT haiwezi kuendeshwa na serikali peke yake bila ya wadau wa maendeleo, hivyo kampuni ya Kahama Fresh imeunga mkono programu hiyo kwa vitendo.

Alisema kitendo hicho kitatoa hamasa kwa wadau wengine kujitokeza.

Waziri Ulega aliwakikishia wadau kuwa

wataendelea kushirikiana nao programu hiyo ya kielelezo ya BBT ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan ishamiri na vijana wengi wapate fursa za kujijiri.

Mkurugenzi wa Kampuni hiyo, Ntangeki alishukuru serikali kwa kuendelea kuwapa fursa ya kuendesha shughuli zao.

Alisema wametoa mitamba hiyo kuunga mkono jitihada za Rais Samia za kuwawezesha vijana kupata fursa mbalimbali za kujijiri kupitia sekta za uzalishaji.

Kahama imetoa ng'ombe hao kupitia programu Kopa Ng'ombe Lipa Maziwa unaotekelezwa na Shirika la kimataifa la Heifer International kupitia mradi wa kuboresha sekta ya maziwa (TISP) kwa Kanda ya Ziwa na Zanzibar.

Mradi huo unafadhiliwa na Taasisi ya Bill and Melinda Gates (BMGF) kupitia Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB).

Utoaji ng'ombe watano kwa vijana ni sehemu ya uzinduzi wa mpango wa ukopeshaji ng'ombe 600 watakaotolewa na TADB kupitia programu ya Kopa Ng'ombe Lipa Maziwa.

UZINDUZI MPANGO

Utoaji ng'ombe watano kwa vijana ni sehemu ya uzinduzi wa mpango wa ukopeshaji ng'ombe 600 watakaotolewa na TADB kupitia programu ya Kopa Ng'ombe Lipa Maziwa.

HABARI LEO UK 5.

Kahama Fresh yatoa mitamba BBT, TADB yaipa bil 1/-

Na Mwandishi Wetu,
Karagwe

BENKI ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) imetoa Sh bilioni 1.7 kwa ajili ya kununua ng'ombe mitamba 600 kuunga mkono juhudi za mwekezaji wa kiwanda cha maziwa cha Kahama Fresh katika mradi wake wa 'Kopa Ng'ombe Lipa Maziwa' ili kuwawezesha vijana kujiajiri.

Mkurugenzi wa TADB, Frank Nyabundege alisema kuwa serikali ilikuja na maono ya mradi wa BBT Jenga kesho yako iliyo njema kwa sekta ya uvuvi na mifugo na mwekezaji huyo akatumia maono hayo kujenga kesho ya vijana wafugaji katika Wilaya ya Karagwe.

Katika hatua nyingine kampuni ya Kahama Fresh inayomiliki kiwanda cha kusindika maziwa na shamba la mifugo, imeunga mkono programu ya BBT kwa kutoa ng'ombe wa maziwa watano kwa kikundi cha vijana 17 ili kuwawezesha kujishughulisha na uzalishaji wa maziwa na kujiongezea kipato.

Hafla ya makabidhiano hayo imefanyika katika

shamba la mifugo la kampuni hiyo lililopo wilayani Karagwe mkoani Kagera juzi.

Akizungunza wakati wa kukabidhi ng'ombe hao kwa vijana, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega alimpongeza Mkurugenzi wa Kahama Fresh, Josam Ntangeki kwa kuunga mkono BBT kwa vitendo.

Alisema programu hiyo ya BBT haiwezi kuendeshwa na serikali peke yake bila ya wadau wa maendeleo, hivyo Kampuni ya Kahama Fresh imeunga mkono programu hiyo kwa vitendo.

Mkurugenzi wa Kampuni ya Kahama Fresh, Ntangeki aliishukuru serikali kwa kuendelea kuwapa fursa ya kuendesha shughuli zao.

Ntangeki alisema wametoa mitamba hiyo kuunga mkono jitihada za Rais Samia za kuwawezesha vijana kupata fursa mbalimbali za kujiajiri kupitia sekta za uzalishaji ikiwamo mifugo.

Kahama Fresh imetoa ng'ombe hao kupitia Programu ya Kopa Ng'ombe Lipa Maziwa inayotekelezwa na Shirika la Kimataifa la Heifer International kupitia Mradi wa Kuboresha Sekta ya Maziwa